



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuelewa Mchakato wa Rufaa na Ustahiki: Mwongozo wa Mzazi

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org





Kuelewa Mchakato wa Rufaa na Ustahiki: Mwongozo wa Mzazi

Mtoto hupatiwaje rufaa ya huduma za elimu maalum?

Rufaa inaweza kufanywa shuleni na:

- Mzazi ama mlezi
- Mwalimu ama mfanyikazi wa shule
- Daktari ama mtaalamu wa kijamii

Unaweza kuomba rufaa kwa njia ya matamshi au kwa maandishi ikiwa unaamini kuwa mtoto wako anaweza kuwa na ulemavu unaoathiri masomo yake. Hii inaanzisha mchakato wa tathmini.

Nini hufanyika baada ya rufaa kuwekwa?

Shule lazima ijibu ile rufaa mara moja. Moja ya mambo mawili yatatokea:

- Shule itaomba ruhusa ya mzazi kumtathmini mtoto, au
- Shule itaandika barua kueleza kwanini haitaendelea mbele

Shule iko na siku 60 za kalenda baada ya kupokea idhini iliyoandikwa kukamilisha tathmini na, ikiwezekana, kufanya mkutano kuunda Mpango wa Elimu wa Mtu Binafsi (IEP).

Tathmini ni nini?

Tathmini ya kina hukusanya taarifa kuhusu vile mtoto wako anavyojifunza, kutenda, na kuingiliana. Lengo ni kuelewa uwezo na mahitaji ya mtoto wako katika maeneo mbalimbali. Inaweza kujumuisha:

- Tathmini za Kitaaluma
- Upimaji wa kisaikologia ama tabia
- Uchunguzi
- Maoni kutoka kwa waalimu na wazazi





Wataalamu peke yao, kama vile mwanasaikologia wa shule, mtaalamu wa hotuba na lugha, au mwalimu, anaruhusiwa kufanya tathmini.

Tathmini itafanyika katika lugha gani?

- Tathmini lazima zifanyike katika lugha ambayo(zo) mtoto anaelewa vizuri.
- Mahojiano na wazazi pia lazima yafanyike katika lugha ambayo(zo) wazazi wanaelewa vizuri.

Je, wazazi wanahitaji kupeana ruhusu ya tathmini?

Ndio. Shule lazima iwe na idhini iliyoandikwa na mzazi au mlezi kabla ya kuanza tathmini. Wazazi wanahimizwa kuuliza maswali ili kuelewa kitakachojumuishwa kwenye tathmini.

Nini hufanyika baada ya tathmini?

Tathmini inapokamilika, mkutano huitwa kujadili matokeo. Timu inaamua iwapo mtoto ako na ulemavu ama hana. Mkutano huo unaitwa mkutano wa kustahiki.

Je, ni nani anayeamua kama mtoto anastahiki?

Timu ya kustahiki inajumuisha:

- Mzazi(wazazi) au Mlezi(walezi) wa mtoto
- Walimu wa kawaida au wa elimu maalum
- Mwanasaikolojia wa shule au watathmini wengine
- Msimamizi wa shule

Timu inachunguza matokeo yote na kukubaliana kama mtoto anastahiki.





Nini kinafanyika ikipatikana kuwa mtoto anastahiki?

Shule lazima iunde IEP. Mpango huo unaeleza malengo, huduma, na jinsi maendeleo yatakavyopimwa.

Je, ikiwa mtoto hastahiki?

Timu itaeleza uamuzi na kutoa hii kwa maandishi. Pia itapendekeza njia zingine za kumsaidia mtoto kando na huduma za elimu maalum.

Je, Mzazi asipokubaliana na matokeo ya tathmini, ni nini kitakachofanyika?

Usipokubaliana, unaweza:

- Kuomba mkutano kujadili wasiwasi wako
- Kuitisha tathmini nyingine kutoka kwa wahusika wengine
- Kuweka lalamishi rasmi au kuomba upatanishi au kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa

Wazazi wanahusikaje kwenye mchakato?

Wazazi ni washirika muhimu kwa wakati wote. Una haki ya:

- Kuwa na taarifa na kutoa maoni
- Kutoa au kuzuia idhini ya tathmini na huduma
- Kuomba tathmini au mikutano ya IEP
- Kukagua rekodi na uulize maswali wakati wowote

Bado una maswali?

Ongea na mratibu wa elimu maalum wa shule yako au mkuu wa shule. Unaweza pia kuwasiliana na Kituo cha Mafunzo na Taarifa kwa Wazazi (PTI) cha jimbo lako kwa usaidizi bila malipo.





Nawezaje kupata usaidizi kwa lugha yangu?

Omba huduma za mkalimani katika shule ya mtoto wako ama katika ofisi za wilaya ya shule. Omba taarifa zilizotafsiriwa na kuandikwa iwapo unazihitaji. Taarifa zizonapatikana kwa wazazi wote katika wilaya ya shule zinafaa kupatikana kwako pia.

